



KUONGEZA MUDA WA UPOKEAJI MAOMBI YA UFADHILI WA MASOMO YA SHAHADA YA KWANZA MWAKA 2017/18

Mfuko wa Udhamini wa Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Nyerere unaosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), unatangaza kuongeza muda wa kupokea maombi ya ufadhili kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu kwa Shahada ya Kwanza.

Kutokana na baadhi ya wanafunzi kuwa bado kwenye Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa mfuko utaendelea kupokea maombi kwa ajili ya ufadhili wa masomo ya Shahada ya Kwanza hadi tarehe 15 Septemba, 2017.

Mfuko wa Udhamini wa Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Nyerere ulianzishwa na BoT mwaka 2009. Unalenga kuongeza hamasa na ufaulu kwa wanafunzi wa kike hapa nchini katika **masomo ya Hisabati na Sayansi**. Ufadhili unajumuisha gharama zote za ada, pesa za kujikimu, mafunzo ya vitendo na vifaa vya kujifunzia, ikiwemo kompyuta mpakato (Laptop).

Kwa Shahada ya Kwanza, ufadhili utatolewa kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu – yaani Daraja la Kwanza miongoni mwa wanafunzi kumi bora kitaifa wa kidato cha sita mwaka 2017, kwa masomo ya Hisabati na Sayansi kwa wanafunzi wa kike na masomo ya Uchumi, TEHAMA, Uhasibu na Fedha kwa wanafunzi wa kike na wa kiume.

Fomu za Maombi kwa ajili ya Udhamini huu zinapatikana katika Tovuti ya Benki Kuu: www.bot.go.tz. Fomu pia zinapatikana Benki Kuu Makao Makuu na katika Matawi ya Benki (Mwanza, Arusha, Zanzibar, Mbeya, Dodoma na Mtwara).

